

Taarifa ya mwaka 2009: **KWA UFUPI**

Mkombozi

SLP 9601
Moshi, Tanzania
Moshi tel: +255 27 2754793
Arusha tel: +255 272544319
info@mkombozi.org
www.mkombozi.org

Yaliyomo

uk.3 Ujumbe kutoka Mwenyekiti wa bodi ya wathamini
uk.4 Ulinzi
uk.5 Elimu
uk.6 Uwezeshaji
uk.7 Ushirikishaji
uk.8 Kujifunza
uk.9 Uvumbuzi
uk.10 "Katika maneno yao"
uk.11 Taarifa ya Fedha 2009

Imehaririwa & kuandaliwa na Tanja Kisslinger; Picha na Anna Thor

© 2010 Mkombozi

Mkombozi ni Asasi ya Dhamana Iliyosajiliwa Tanzania (ADP / P12097)

Marafiki wa Mkombozi Asasi ya Msaada Iliyosajiliwa Uingereza (1101318)

Mkombozi ni nini?

Mkombozi ni shirika linalofanya kazi kuwasaidia watoto na vijana kukua kiakili, kimwili na kiroho. Tunataka kujenga jamii ambayo kila mmoja anamjali mwingine. Ndoto ya Mkombozi ni kuwa na dunia ambapo watu wote wanawapa umuhimu watoto na vijana - dunia ambapo vijana wanapata elimu, wanaishi maisha mazuri na wanafanya kazi kuendeleza jamii zao.

Mkombozi inasaidia watoto na vijana wa aina gani?

- Watoto na vijana wasio na makazi na wanaolala mitaani.
- Watoto wanaoamua kuishi au kufanya kazi mitaani.
- Watoto wanaokwenda mjini kuombaomba au kufanya kazi mchana na kurudi nyumbani usiku.
- Watoto wanaochukuliwa kutoka nyumbani kwao na kuletwa mjini kutumiwa na watu wazima.
- Watoto walio katika hali ngumu sana manyumbani mwao.
- Watoto na vijana wanaojishughulisha na biashara ya ngono ili kujikimu kimaisha.

Nini maana ya "Taarifa ya mwaka 2009: KWA UFUPI"?

Mkombozi huandika "taarifa ya mwaka" kuonyesha utekelezaji wa shughuli na mafanikio kila mwaka. Kijitabu hiki ni muhtasari wa Taarifa kamili ya Mwaka 2009; ni toleo fupi na rahisi kwa wale ambao wanapenda kuipitia kwa haraka taarifa kamili. Muhstasari huu hutusaidia sisi kutoa taarifa ya shughuli na mafanikio yetu kwa watu wengi zaidi. Tafadhali furahia muhstasari huu wa kazi za Mkombozi kwa mwaka wa 2009 na baadhi ya matukio muhimu yaliyojiri katika mwaka huo.

Ujumbe kutoka Mwenyekiti wa bodi ya wathamini

2009 ulikuwa mwaka wa kuimarisha maono na malengo yetu, kujenga mawazo kwa ajili ya siku za mbeleni pamoja na timu thabiti za kiutendaji. Pia ulikuwa ni wakati wa Mkombozi kurejea katika shughuli zake kuu. William Raj alijiimarisha katika majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji kwa kujiamini akiwa tayari kwa mabadiliko.

Mkombozi ilianza kuweka mpango wa miaka mitano ijayo. Kuweka Mpango huo kulileta tafakari nzuri ambayo itaifanya Mkombozi kuendelea kuwasaidia watoto kukua kiakili, kimwili na kiroho - pamoja na kuitia hamasa jamii ili kuwajibika kwa watoto. Katika mchakato huu Mkombozi ilihakikisha kwamba wadau wote wanapata fursa ya kueleza mahitaji na maslahi yao.

Mkombozi yaendelea kuwezesha jamii kuwajibika katika malezi ya watoto kupitia miradi mbalimbali. Haya yamefanyika kwa vigezo vya tafiti na uzoefu ambavyo vinaonesha kwamba kuwaweka watoto kwa muda mrefu katika kituo kunawanyima fursa ya kukua sawasawa kijamii na kiutamaduni.

Mkombozi ilinunua ardhi katika kata ya Sambarai, wilaya ya Moshi Vijijini, na ina mpango wa kujenga Kituo Cha Kulinda Haki za Watoto na Jamii hapo. Huko mbeleni, watoto ambao hukimbia nyumbani wakitafuta maisha bora mitaani wataweza kurejea nyumbani kirahisi kwa kupitia katika kituo hiki.

Huu ulikiwa mwaka wa tafakari na kukua, na ninasikia heshima kuwa sehemu ya Mafanikio Endelevu ya Mkombozi.

Kara Kirby

Vijengea MAFANIKIO:

- Ulinzi
- Uwezeshaji
- Ushirikishaji
- Elimu
- Kujifunza
- Uvumbuzi

Mkombozi inathamini ulinzi kwa mtoto na kijana kwa sababu watoto wanaweza tu kukua kikamilifu endapo watalindwa na hatari.

Mambo muhimu kwa ufupi kuhusu ULINZI ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2009...

- Vijana 766 (kati ya wavulana 686 na wasichana 80) walipata huduma toka Mkombozi.
- Milo 49,735 ilitolewa kwa watoto na vijana kituoni Mkombozi.
- Wavulana 79 na msichana 1 walipata malazi kituoni Mkombozi.
- Vipindi 49 vya masomo ya Elimu ya Afya vilitolewa.
- Huduma za Afya zilitolewa mara 3,572 kwa watoto na vijana.

Kesi ya Mkombozi yashindwa Mahakama Kuu: Nchini Tanzania, kuna sheria ambazo huruhusu Mamlaka za Serikali kuwashika na kuwaweka gerezani vijana kwa sababu ya kuishi mitaani. Lakini hili ni kinyume cha Haki za Watoto, na lina madhara kwa watoto. Mkombozi na wanachama wengine wa Caucus for Children's Rights (CCR), kwa muda, wamekuwa na kesi Mahakama Kuu ya Tanzania wakisihi kuondolewa kwa sheria hizi. Tunasikitika kutangaza kwamba kesi hii haikuwa na mafanikio - Mahakama iliamua kwamba ni kwa maslahi ya umma endapo watoto wanaoishi/kufanya kazi mitaani wataondolewa. Mwaka 2010, CCR inakata rufaa kupinga uamuzi wa mahakama.

"Sheria ya Mtoto!" - Sasa Tanzania ina sheria kwa ajili ya haki za Watoto: Kama miaka 20 hivi, Tanzania ilitoa ahadi ya kuweka sheria ya Haki za Watoto na kubadilisha sheria za nchi iliporidhia Azimio la Haki za Watoto (CRC). Kutoka hapo asasi za kiserikali na zisizo za kiserikali zimekuwa zikiandaa rasimu ya sheria mpya. Mnamo mwaka 2009, kundi la mashirika (Mkombozi ikiwa mwanachama) lilishawishi serikali kutunga Sheria ya Mtoto - jambo ambalo lilikamilika pale ambapo sheria hii ilipitishwa na bunge pamoja na raisi mwishoni mwa mwaka. Pamoja na mambo mengi, Sheria ya Mtoto huwapa watoto wote haki ya kulindwa dhidi ya unyanyasaji na kutumikishwa, na huweka bayana majukumu ya wazazi.

Muuguzi wa Mkombozi akimpima shinikizo la damu mtoto anayeishi kituoni Mkombozi.

Mkombozi inathamini elimu kwa sababu huwawezesha vijana walio katika mazingira magumu fursa ya kujiendeleza na kujitegemea.

Mambo muhimu kwa ufupi kuhusu ELIMU ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2009...

- Wavulana 322 na wasichana 3 walishirki katika elimu itolewayo mtaani kupitia Mobile School na Mobile Unit.
- Wavulana 46 na msichana 1 walisoma katika madarasa ya MEMKWA kituoni Mkombozi.
- Vijana 18 waliandikishwa katika mfumo wa elimu rasmi baada ya kuhudhuria madarasa ya MEMKWA kituoni Mkombozi.
- Wasichana 13 na wavulana 88 waliwezeshwa kusoma elimu ya msingi, sekondari na vyuo.

Watoto 47 walisoma kituo cha MEMKWA Mkombozi: MEMKWA ni mpango wa kiserikali wa kuwawezesha watoto ambao hawako shuleni wawafikie wenzao ili waingie shule ya msingi. Mkombozi huendesha madarasa ya MEMKWA kwa lengo la kuwezesha kurejesha watoto shuleni, na kutafiti zaidi juu ya hali zao hasa baada ya kuishi mitaani. Kwa baadhi, Mkombozi huendesha madarasa ambayo hatimaye huwawezesha kujifunza kusoma na kuandika. Tausi, msichana ambaye hakuwahi kusoma, alisema yafuatayo baada ya kuhudhuria madarasa ya MEMKWA mwaka 2009: "Sasa naona mabadiliko makubwa, kwa sababu sasa naweza kusoma na kuandika mambo, na watu wanaweza kuelewa nilichoandika. Na endapo nikiona tangazo au alama inayoniashiria kitu cha kufanya au nisifanye, naelewa."

Watoto na vijana waibua vipaji vyao: Kuwapa fursa watoto waibue vipaji vyao ni sehemu muhimu ya kazi za Mkombozi kwa sababu huwasaidia kukua vema. Mwaka 2009, Shirika la "Cre8 East Africa" liliwapa watoto wa Mkombozi pamoja na wenzao toka kwenye jamii mafunzo ya sanaa ya muziki wa ubunifu. Pia vijana kutoka Mradi wa Kiholanzi "Change Beats" walikuja kutayarisha muziki pamoja na vijana wa Mkombozi. Charles, mmoja wa washiriki katika mafunzo ya Cre8 alisema hilo juma lilimsaidia: "[....] Kujiamini, kulimudu jukwaa, na kutokuwa na hofu yoyote nisimamapo mbele ya watu. Kabla ya hapo, nilikuwa mwoga, lakini Cre8 ilinisaidia kujiaminisha mwenyewe, kujiamini na kugundua mambo mengi."

Mwanagenzi wa mafunzo ya kompyuta akipata ujuzi ACTT ambao utamjengea mafanikio katika teknologia ya habari (IT).

Uwezeshaji

Mkombozi inathamini uwezeshaji wa vijana kwa sababu watoto na vijana hukua vema wanapoyamudu na kuwajibika juu ya maisha yao wenyewe.

Mambo muhimu kwa ufupi kuhusu UWEZESHAJI ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2009...

- Wavulana 35 na wasichana 3 waliunganishwa na familia zao.
- Ziara 191 zilifanywa katika familia au nyumbani kwa watoto na vijana.
- Wasichana 4 walihamia Mfumo wa Kukaa katika Nyumba za Mpito (Transitional Housing).
- Vijana 4 waliunganishwa kwenye nafasi za ajira.

Kituo cha Kukaa Mkombozi kuwa cha Muda: Mkombozi imeanza kukibadilisha kituo cha kukaa kutoka kituo cha watoto kukaa muda mrefu kuwa makazi au mahali pa au kukimbilia kwa muda kwa watoto/vijana ambao wanahitaji msaada wa ulinzi. Kwa sasa Mkombozi inafanya kazi ya kuchunguza/kuona endapo mtoto/kijana mgeni anaweza kurudi nyumbani au kuishi na na mtu katika jamii. Kwa kuwa watoto/vijana waliowahi kuishi kituoni Mkombozi walionyesha kuwa maisha kituoni Mkombozi hayakuwaandaa waweze kuishi maisha ya kujitegemea katika jamii, Mkombozi ilielekeza juhudi zake kwa mwaka 2009 katika kuwawezesha kurejea nyumbani au waanze maisha ya kujitegemea. Mvulana mdogo aitwaye Immanuel, ambaye aliunganishwa na shangazi yake mwishoni mwa mwaka alisema mambo yafuatayo kuhusiana na maisha pale Mkombozi: "Ninafurahi sana kwa sababu ninalala kwa raha, na sasa ninajua kusoma na kuandika kidogo. Napenda kucheza mpira wa mguu na nafurahia kula wali na tambi. Nina afya njema sasa, na ninakula kila siku.Nilipokuwa naishi na kaka yangu tulikuwa tunaokota chuma chakavu [tuuze ili kujikimu kimaisha], na endapo hatukuokota chochote basi siku hiyo tusingekula".

Mkombozi yashirikiana na ofisi ya Ustawi wa Jamii Mkoa wa Kilimanjaro: Kwa kupitia ubia wake na Ofisi ya Ustawi wa Jamii mkoa wa Kilimanjaro, Mkombozi iliongeza mafanikio katika kuwaunganisha watoto na familia zao, kuwawezesha vijana kujitegemea, na kuhusisha mamlaka za kiserikali. Kuanzia mwaka 2009, Afisa Ustawi wa Jamii hufanya kazi na Mkombozi kila juma katika kuhakikisha kwamba watoto na vijana ambao wamekuwa mtaani wanarejea katika jamii zao, na kwamba wao pamoja na familia zao wanafahamu majukumu yao.



Mkutano wa wazazi katika Shule ya Msingi Mji Mpya iliyoko Moshi Mjini.

Mkombozi inathamini ushirikishaji wa jamii kwa sababu huboresha hali ya watoto kunategemea mabadiliko katika jamii na serikali.

Mambo muhimu kwa ufupi kuhusu USHIRIKISHAJI ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2009...

- Wavulana 3 kutoka kituo cha malezi Mkombozi walikaa na familia za kulea/rafiki wakati wa sikukuu ya Krismasi.
- Vijana 7 toka kituoni na vijana 27 toka kwenye jamii waliunganishwa na Kaka/Dada Mkubwa.
- Walezi 14 na Kaka/Dada Wakubwa 6 walijitolea katika Shule ya Msingi Rau.
- Vijana 5 walianza masomo kama wanagenzi wa mafunzo ya kumputa ACTT.

ACTT yaeneza Teknologia ya Habari na Mawasiliano Kanda ya Kaskazini: Katika kipindi cha mwaka uliopita, ACTT (Mradi wa Mkombozi unaozalisha) iliendelea kutumia Teknologia ya Habari na Mawasiliano (ICT) kuwawezesha vijana, mashule na jamii nzima - hivyo kuchangia katika maendeleo ya kitaifa. Miongoni mwa juhudi nyingine nyingi, ACTT iliwasaidia vijana watatu katika kuanzisha biashara zao wenyewe ndogo "Banda Business" kuuza bidhaa za Teknologia ya Habari na kutoa huduma katika vituo mbalimbali mijini.

Kuwaelimisha walimu juu ya ulinzi wa Watoto: Mwaka 2009, Mkombozi iliendesha warsha kuhusiana na unyanyasaji na ulinzi wa watoto kwa walimu wa shule nne za kata ya Majengo (Moshi). Iligundulika wakati wa mafunzo kwamba adhabu ya Viboko (bakora) - kitu ambacho Mkombozi hupinga - ni ya kawaida sana. Mkombozi ilipata fursa ya kuwatia moyo walimu wawe mabalozi wa Haki za Watoto, na kuepuka kutumia nguvu katika kushughulikia nidhamu ya watoto.

Mradi wa Kaka/Dada Mkubwa wakua katika Jamii: Kwa kupitia Mkombozi, watu wanaweza kujitolea kama "Kaka Mkubwa" au ""Dada Mkubwa" kumsaidia mtoto ambaye hana msaada wa mtu mzima wa kumwongoza kwa kuwa rafiki yake. Huko nyuma, mpango huu ulikuwepo tu kwa watoto waliokuwa wanakaa kituoni. Katika mwaka 2009, "Kaka/Dada Mkubwa" ilihamia kwenye jamii kwa kuwa watu wengi waliojitolea waliunganishwa na watoto wanaoishi majumbani, na ambao wanasoma Shule ya Msingi Rau, Moshi.

ⓘ Kujifunza

Mkombozi inathamini kujifunza maisha mazima kwa sababu kupitia kujifunza tunaweza kuleta badiliko kwa watoto kwa kuwasikiliza wadau wetu na kutafakari juu ya uzoefu/utendaji wetu.

Mambo muhimu kwa ufupi kuhusu KUJIFUNZA ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2009...

ⓘ Taasisi 12 za kielimu ziliwezeshwa kufanya kazi kama Vituo vya Kiteknologia vya Kujifunzia kwa Jamii (CTLCs).
ⓘ Vijana 3307 walimaliza kozi za Teknologia ya Habari kupitia ACTT na CTLCs.
ⓘ Walimu 59 toka shule nne za Msingi walipata mafunzo ya ulinzi wa Mtoto.
ⓘ Wanajamaii zaidi ya 3000 walihudhuria maigizo yanayohusiana na kuleta mwamko juu ya suala la unyanyasaji wa watoto.

Watoto na Vijana waliridhika na Huduma za Mkombozi: Kila mwaka, Mkombozi hufanya tathmini kuona ni jinsi gani watoto na vijana wanavyoziona huduma zetu. Mwaka 2009, tathmini hiyo ilionesha kwamba kwa ujumla vijana wale tunaofanya nao kazi wanafurahia huduma zetu - hasa kuzingatia utoaji wa huduma ya afya kwa vijana walio mitaani, na heshima na mawasiliano yaliyoko kati yao na wafanyakazi wa Mkombozi.

Mabadiliko ya Msingi katika kujitambua na Uwezo wa kuishi na wengine: Mkombozi huwahimiza wadau kutoa simulizi zenye Mabadiliko ya Msingi Zaidi ambayo yamesababishwa na kujihusisha kwao na Shirika. Kwa mwaka 2009, kwa kuzitazama simulizi hizi kwa undani kulionyesha kuwa watoto na vijana wengi walielezea mabadiliko juu ya uwezo wao wa kuweka mipango ya muda mrefu, kujenga mahusiano na kukubalika katika jamii. Pia wengine walielezea mabadiliko kimtazamo, kimaadili na kitabia. Mvulana mmoja alisema: "Tabia yangu imebadilika, ni tofauti na ilivyokuwa awali, na sasa nimerudi nyumbani na ninaishi vizuri na jamii." Mwingine alisimulia kwamba muda aliokaa Mkombozi, alijifunza; "kuwa na tabia njema na kuwaheshimu wengine." Aliona kuwa hilo ni badiliko la msingi kwa sababu, "Usipomheshimu mwingine, naye hatakuheshimu wewe. Hii itakuletea matatizo, na utarejea mitaani kuhangaika. Heshima na utii ni vya muhimu sana katika maisha ya mtu."

Vijana wa Mkombozi wakishiriki katika Mradi wa Cre8 wa "Kuibua Vipaji" Juni, 2009.

Mkombozi inathamini uvumbuzi kwa sababu badiliko zuri/chanya kwa watoto hutegemea mawazo na matukio ambayo hugeuza namna ambavyo watu hufikiri.

Mambo muhimu kwa ufupi kuhusu UVUMBUZI ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2009...

- Vijana 482 walifikiwa kupitia huduma zetu za mtaani (wavulana 469 na wasichana 13).
- Vijana 140 toka kituoni, mtaani na shuleni walishiriki katika Siku ya Michezo Mkombozi.
- Tulifanya kazi na viongozi wa mitaa katika kata tatu kuunda Kamati za Ulinzi wa Mtoto.
- Wavulana 17 na wasichana 12 walimaliza mafunzo ya Biashara ya Mtaani (SBTK).

Mkombozi ilishiriki katika miradi mbalimbali ya utafiti: Mwaka 2009, Mkombozi ilihusika katika Uchunguzi wa Kitaifa juu ya watoto waishio na kufanya kazi mitaa ya miji saba (ulioongozwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Shirikisho la Wanaojishughulisha na Watoto waishio Mitaani). Pia, Mkombozi ilishiriki katika utafiti uliofanywa na Shirika la Railway Children ambao ulilenga katika kupata uzoefu wa maisha ya watoto mitaani Tanzania na Kenya. Mwisho, tumekuwa tukifanya utafiti kujua kama program za Mkombozi zinaongeza uwezo wa kurejea hali ya awali (yaani Uwezo wao wa kumudu na kuendelea vema ingawa walikumbana na hali ngumu huko nyuma).

Upimaji kuona ufahamu wa watu kuhusiana na watoto waishio mitaani: Kwa kufanya upimaji mdogo wa takriban wanajamii 100, Mkombozi ilipata mengi juu ya nini watu wanachofahamu kuhusiana na watoto wanaoishi mitaani. Upimaji huu ulitufanya tuhisi kwamba kuna ukosefu wa ufahamu katika jamii juu ya watoto wanaoondoka nyumbani kwa sababu ya kunyanyaswa, magomvi katika familia au ukosefu wa matunzo yanayofaa toka kwa wazazi wao. Ulitufanya pia tuone kwamba watu wengi wanadhani kwamba jukumu la watoto walioko mitaani ni la serikali. Mtu mmoja aliyeshiriki katika upimaji huo alisema, "Ningependa serikali, pamoja na makundi mbalimbali ya kidini washirikiane katika kuwakusanya na kutafuta kujua nyumbani kwa watoto wanaoishi mitaani ni wapi, na hapo ndipo watapata sababu kuu iliyowafanya waondoke nyumbani."

Tafakari za Mwaka 2009

> > > MKOMBOZI YAINGIA KATIKA KIPINDI KIPYA > > >

Katika miaka michache nyuma, Mkombozi ilikua kwa haraka sana kama shirika - kwa ongezeko na namna ya kiutendaji pia. Mwaka 2009, ulifika wakati wa kuanza mchakato wa kuweka mpango wa miaka mitano ijayo, mpango ambao utaleta mabadiliko mengi mazuri kwa shirika.

Kwa kutazama mbele, Mkombozi inataka kuwa mashuhuri katika kuwawezesha watoto, na kuzisaidia jamii ili ziweze kuwa hai kiukweli katika kuwajibika kujiletea maendeleo yao wenyewe. Pia, Shirika linataka kuwa na malengo ya kufanya mambo machache ili kwamba liweze kuleta mabadiliko makubwa zaidi katika maisha ya watoto.

Baadhi ya maswali makuu ambayo Mkombozi ilikuwa inajiuliza mwishoni mwa mwaka 2009, kabla ya kuanza Mpango Mkakati, yalikuwa haya yafuatayo...

> Tufanye kazi na watoto/vijana wepi hapo baadaye? Umri wao uwe upi? Je, tuwalenge zaidi wavulana, wasichana au wote? Ni msaada gani unaofaa zaidi ambao tunaweza kuutoa kwa kundi tunaloamua kujishughulisha nalo?

> Tutoe matunzo ya aina gani kituoni? Tuweke ukomo wa muda ambao watoto wanaweza kukaa hapo kabla hawajarejea katika jamii? Watoto wapatiwe huduma gani wawapo kituoni? Ni kwa namna gani tunaweza kuboresha uunganishaji watoto na familia?

> Je, Mkombozi itawezeshaje jamii ili jamii yenyewe iweze kushughulikia masuala ya watoto? Je, namna tunavyotenda kazi inawezaje kuwezeshwa zaidi na hali ya ndani? Tunawezaje kuishawishi serikali na sera zake ili ilinde na kusimamia/tetea haki za watoto?

> Je, Affordable Computers & Technology for Tanzania (ACTT) ijikite zaidi katika kutumia Teknologia ya Habari kuwaweza vijana na jamii zilizo kwenye mazingira magumu? Au iwe na sura ya kibiashara ili iongeze faida ikiwa na malengo ya kuwezesha kazi za Mkombozi na watoto kifedha?

Maelezo ya taarifa za fedha

kwa mwaka uliomalizika 31 Disemba 2009

(Taarifa hizi zimeandaliwa katika shilingi za Ki-Tanzania)

MAPATO

RUZUKU	
Comic Relief	234,215,160
Foundation for Civil Society	125,900,856
Friends of Mkombozi	64,144,750
Railway Children	65,354,868
International Child Support	134,206,200
Research on Poverty Alleviation (REPOA)	7,152,600
Pestalozzi Children's Foundation	111,045,900
Star Foundation	64,544,015
International Organization for Migration	7,470,240
OAK Foundation contribution	8,156,205
DONATIONS	8,169,950
JUMLA YA MAPATO	830,360,744

MATUMIZI

PROGRAMMES	-816,130,819
ACTT	43,321,217
Other	- 11,663,038
JUMLA YA MATUMIZI	784,472,640

Mkombozi

SLP 9601
Moshi, Tanzania
Moshi tel: +255 27 2754793
Arusha tel: +255 272544319
info@mkombozi.org
www.mkombozi.org